# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

# MWONGOZO WA KURATIBU USHIRIKI WA WADAU WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM KATIKA MIKUTANO YA KIKANDA NA KIMATAIFA

JUNI, 2024

## YALIYOMO

YALIYOMO .......... i
VIFUPISHO .......... iii
TAFSIRI YA MANENO .......... iv
SHUKRANI .......... vi
DIBAJI .......... vii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .......... 1
1.1. Maelezo ya Awali .......... 1
1.2. Dhana na Ufafanuzi wa Mwongozo .......... 2
1.3. Malengo ya Mwongozo .......... 3
1.3.1. Lengo Kuu .......... 3
1.3.1.1. Malengo Mahsusi .......... 3
1.3.1.2. Walengwa wa Mwongozo .......... 3
1.3.1.3. Umuhimu wa Mwongozo .......... 4
SURA YA PILI: CHIMBUKO NA MSINGI WA KISHERIA .......... 5
2.1 Chimbuko .......... 5
2.2 Hali Ilivyo Sasa .......... 5
2.3 Msingi wa Kisheria .......... 6
SURA YA TATU: URATIBU NA UTOAJI WA TAARIFA .......... 7
3.1 Utangulizi .......... 7
3.2 Utaratibu wa Ushiriki wa Mikutano .......... 7
3.2.1 Masuala ya kuzingatia kabla ya kufanyika Mkutano .......... 7
3.2.2 Masuala ya kuzingatia wakati wa Mkutano yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa .......... 8
3.2.3 Masuala ya Kuzingatia baada ya Mkutano: - .......... 8
3.2.4 Masuala mengine muhimu yatakayozingatiwa wakati wa ushiriki wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa kwa washiriki ni kama ifuatavyo;9
SURA YA NNE: WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU .......... 10
4.1 Wajibu wa Serikali .......... 10
4.2 Wajibu wa Wadau .......... 10
4.2.1 Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na makundi Maalum .......... 10

4.2.2 Wizara yenye dhamana ya Itifaki ya Kikanda na Kimataifa itakua na majukumu yafuatayo ........ 11
4.2.3 Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ........ 11
4.3 Majukumu ya Wadau Wengine ........ 12
Majukumu yao ni kama ifuatavyo: - ........ 12
SURA YA TANO: URATIBU NA TATHIMINI ........ 13
5.1 Utangulizi ........ 13
5.2 Uratibu ........ 13
5.1.1 Muundo wa Sekretarieti ........ 13
5.1.2 Majukumu ya Sekretarieti ........ 13
5.2 Tathmini ........ 14
SURA YA SITA: HITIMISHO ........ 15

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ACRWC | African Charter on the Rights and Welfare of the Child |
| CEDAW | Convention on the Elimination of All Forms of Discrimination Against Women |
| CRC | Convention of the Rights of the Child |
| CSW | Commission on the Status of Women |
| SDG | Sustainable Development Goal |
| UNGAs | United Nations General Assembly |

## TAFSIRI YA MANENO


| | | |
|---|---|---|
| 1 | Wadau | Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, Sekta na Watu Binafsi pamoja na Wadau wengine watakaoshiriki kwenye Mikutano hiyo. |
| 2 | Wizara yenye dhamana ya Itifaki ya Kikanda na Kimataifa | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki |
| 3 | Wizara yenye Dhamana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum |
| 4 | Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| 5 | Jinsia | Dhana inayoonesha mahusiano yanayojengwa na jamii ili kutofautisha kati ya wanaume na wanawake. Mahusiano hayo yanagawa majukumu na haki tofauti kwa kila jinsi kutegemeana na utamaduni, mila na desturi |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Makundi Maalum | Ni kundi inayojumuisha wafanyabiashara ndogondogo (Machinga, waendesha bodaboda, waendesha bajaji, baba na mama lishe na wasusi), wajane, wazee, watoto na watu wenye ulemavu |

## SHUKRANI

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum inatoa shukrani za dhati kwa Wadau wote walioshiriki katika uandaaji wa Mwongozo huu. Kipekee, Wizara inatoa shukrani kwa Wadau mbalimbali wanaoshirikiana na Wizara katika kuiwakilisha Nchi kwenye Mikutano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa. Mikutano hiyo ni pamoja na mkutano wa *Women Deliver (2023)* uliofanyika tarehe 17 – 20 Julai, 2023 Kigali Rwanda, Mkutano wa *United Nations General Assembly* **(UNGAs 78)** uliofanyika tarehe 18 – 22 Septemba 2023 Jijini New York na Mkutano wa Kamisheni ya Hali ya Wanawake Duniani *(Commission on the Status of Women –* ***CSW****)* uliofanyika tarehe 11 - 22 Machi 2024 Jijini New York. Ushiriki wa wadau mbalimbali umewezesha kujenga taswira nzuri ya Tanzania na kuwa kama nchi ya kuigwa katika kuimarisha ushirikiano baina ya wadau na Serikali. Vilevile, ushiriki wa wadau umechangia kufanya maandalizi ya pamoja ikiwemo kuandaa taarifa ya Nchi kwa ajili ya kuiwasilisha katika mikutano hiyo.

Ni matumaini yangu kuwa, ushirikiano huu na moyo wa kujituma ulioonekana wakati wa ushiriki na uandaaji wa mwongozo huu utadhihirika wakati wote wa utekelezaji ili kupata matokeo Chanya katika kushiriki Mikutano hiyo.



Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

## DIBAJI

Ushiriki wa Wadau kwenye Mikutano ya Kikanda na Kimataifa unalenga kuimarisha mahusiano baina ya Wadau, Taasisi na nchi kwa ujumla na kutoa fursa kueleza mafanikio na changamoto zinazolenga kuimarisha jitihada za kufikia usawa wa kijinsia. Mwongozo huu unaelekeza mazingira ya utaratibu wa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya ushiriki wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayofanyika ndani na nje ya nchi inayohusu masuala ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika sekta mbalimbali. Pia Mwongozo huu unalenga kutoa maelekezo yatakayowezesha uboreshaji wa namna ya ushiriki wa Mikutano hiyo.

Kwa kuzingatia maelekezo yaliyopo katika Mwongozo huu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Makundi Maalum inaamini kwamba, ushiriki wa Mikutano utafanyika katika ubora uliokusudiwa ili kuleta matokeo chanya yanayolinda maadili ya Kitanzania. Wadau wote watapaswa kuzingatia mwongozo katika kuongeza mashirikiano kati ya wizara na Wadau katika kuratibu Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ili kuwepo na viwango vinavyotarajiwa vya ushiriki na utoaji wa taarifa kwenye Mikutano hiyo.

Dkt. Seif A. Shekalaghe

**KATIBU MKUU - WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM**

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1. Maelezo ya Awali

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia na kusaini mikataba mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa katika kuimarisha haki na ustawi wa wanawake na watoto. Mikataba hiyo ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) 1989, Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (ACRWC) 1990, Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW) 1979, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) 2015, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika Tuitakayo (2063). Kupitia mikataba hiyo, imewezesha Serikali kushiriki katika Mikutano mbalimbali inayotekeleza makubaliano hayo.

Serikali imekuwa ikishirikiana na Wadau katika Mikutano ya ana kwa ana na kwa njia ya mtandao yenye lengo la kuimarisha ushiriki wa Wadau katika kutekeleza mikataba na makubaliano mbalimbali ambayo Serikali imeridhia. Ushiriki wa Wadau katika Mikutano hiyo imekuwa chachu katika kusaidia utekelezaji wa makubaliano hayo katika nchi yetu.

Ushiriki wa Wadau katika ziara za vikao na Mikutano ya Kikanda na Kimataifa imeonesha uwepo wa changamoto mbalimbali ikiwemo Wadau kushiriki Mikutano inayohusu masuala ya Maendeleo ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum bila kushirikisha Wizara yenye dhamana hivyo, kupunguza ufanisi wa uratibu na taarifa kwa Wadau wanaoshiriki Mikutano hiyo.

Hivyo, katika kuimarisha ushiriki wa Wadau, Wizara imeandaa mwongozo huu utakaoboresha ushiriki wa Wadau katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa. Aidha, mwongozo huu umeandaliwa kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uratibu wa ushiriki na Mikutano inayofanyika Kikanda na Kimataifa inayohusu masuala ya maendeleo ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kufanya upembuzi yakinifu kabla ya ushiriki wa nchi katika Mikutano husika. Vilevile, mwongozo huu utaimarisha ushirikiano baina ya Wizara yenye dhamana na Masuala ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara yenye dhamana ya Itifaki ya Kikanda na Kimataifa, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia kwa lengo la kuweka utaratibu katika ushiriki wa Wadau kabla, wakati na baada ya Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ndani na nje ya nchi.

## 1.2. **Dhana na Ufafanuzi wa Mwongozo**

Mwongozo huu unatoa ufafanuzi wa uratibu na ushiriki wa Wadau mbalimbali kwenye ziara za Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ikiwa na lengo la kuimarisha uratibu wa Mikutano kwa kuzingatia usimamizi, uwazi na uwajibikaji wa Mikataba, Makubaliano na Maazimio ya Kikanda na Kimataifa, utekelezaji wa matakwa ya mwongozo huu utakwenda sambamba na utekelezaji wa sheria, taratibu, kanuni na miongozo mingine inayohusu ushiriki wa nchi katika masuala ya kimataifa.

### 1.3. **Malengo ya Mwongozo**

Malengo ya mwongozo huu yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ambayo ni lengo kuu na malengo mahsusi.

#### 1.3.1. **Lengo Kuu**

Kuweka utaratibu wa usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa ushiriki wa Serikali na Wadau mbalimbali katika Mikutano ya nje ya nchi inayohusu masuala ya Maendeleo ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

##### 1.3.1.1. **Malengo Mahsusi**

i. Kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Wadau katika ushiriki wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;
ii. Kuwashirikisha Wadau katika uandaaji na utoaji taarifa za Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;
iii. Kufuatilia na kutathmini ushiriki wa Wadau kwenye Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;
iv. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa maazimio ya mikutano ya Kikanda na Kimataifa; na
v. Kuainisha masuala ya kuzingatia kwenye ushiriki katika Mikutano hiyo ndani na nje ya Nchi.

##### 1.3.1.2. **Walengwa wa Mwongozo**

Walengwa wa mwongozo huu ni Wizara mbalimbali, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi za Kiraia, Taasisi za Dini, na Watu

Binafsi pamoja na Wadau wengine watakaoshiriki kwenye Mikutano hiyo.

### 1.3.1.3. **Umuhimu wa Mwongozo**

Mwongozo huu utasaidia: -

i. Kuimarisha usimamizi, uwazi na uwajibikaji wa masuala ya haki na usawa wa kijinsia na uwezeshaji Wanawake na Makundi Maalum;
ii. Kuongezeka kwa mashirikiano kati ya Wizara na Wadau katika kuratibu Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;
iii. Kupatikana kwa mfumo jumuishi wa uratibu wa kutekelezaji wa masuala ya Maendeleo ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ndani na nje ya nchi;
iv. Kubainisha changamoto, kuzijadili na kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu;
v. Kuongeza upatikanaji wa fursa, uhusiano na ushirikiano uliyotokana na ushiriki wa mkutano husika;
vi. Kuongeza msukumo wa utekelezaji wa maazimio; na
vii. Kulinda maadili ya nchi.

# SURA YA PILI: CHIMBUKO NA MSINGI WA KISHERIA

## 2.1 Chimbuko

Chimbuko la mwongozo huu linatokana na ushiriki wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa Women Deliver uliofanyika tarehe 17- 20 Julai, 2023 Kigali, Rwanda, ambapo ujumbe wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uliongozwa na Mhe. Dkt. Dorothy O. Gwajima (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalum aliyemwakilisha **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo baada ya vikao mbalimbali vilivyoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Dorothy O. Gwajima, ilibainika kuwepo kwa mapungufu katika uratibu wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa iliyopelekea Wadau kukubaliana kuandaa mwongozo huu.

## 2.2 Hali Ilivyo Sasa

Serikali imekuwa ikishiriki katika mikutano mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambapo wadau mbalimbali pia hushiriki. Katika baadhi ya mikutano hiyo kumekuwepo na changamoto mbalimbali ikiwemo:

i. Tofauti ya Taarifa ya Serikali na Taarifa ya Wadau;

ii. Kufanyika kwa mikutano ya pembeni (Side events) bila Wizara yenye dhamana kuwa na taarifa; na

iii. Kutokuwa na maandalizi ya pamoja ya ushiriki wa Nchi.

## 2.3 Msingi wa Kisheria

Msingi wa Mwongozo huu ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara), Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001), Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008), Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake Toleo (2023), Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Sura ya 56 na Sheria ya Mtoto, Sura ya 13 pamoja na Muundo wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (2022) inayoipa Wizara mamlaka ya kuratibu shughuli zote zinazohusu Masuala ya Maendeleo ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

# SURA YA TATU: URATIBU NA UTOAJI WA TAARIFA

## 3.1 Utangulizi

Mwongozo huu umeainisha uratibu na utoaji wa taarifa kwa Wadau watakaoshiriki katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa kwenye Wizara yenye dhamana na Masuala ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Aidha, kuelekea Mikutano ya Kikanda na Kimataifa Wizara yenye dhamana itaratibu uandaaji wa ratiba ya vikao vya maandalizi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki pamoja na Wadau wengine.

## 3.2 Utaratibu wa Ushiriki wa Mikutano

Vikao au Mikutano yote ya ndani na nje ya Nchi inapaswa kuratibiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Katika kutekeleza hilo kila Taasisi, Shirika na mtu binafsi atapaswa kufanya yafuatayo:

### 3.2.1 Masuala ya kuzingatia kabla ya kufanyika Mkutano

i. Kuratibu vikao vya maandalizi katika ngazi ya Makatibu Wakuu na Mawaziri kabla ya ushiriki katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa katika kuleta uelewa wa pamoja;

ii. Ratiba ya Mikutano kwa mwaka mzima itayarishwe na wadau na kuiwasilisha kwenye Wizara yenye dhamana kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji;

iii. Taarifa itakayowasilishwa kwenye Mkutano, iwasilishwe Wizarani na Wadau, na ioneshe muda na malengo ya ushiriki kwenye Mkutano huo;

iv. Kuandaa shughuli zitakazofanyika wakati wa Mkutano kwa kuzingatia mpango wa Wizara/Taasisi; na
v. Wizara kuratibu maandalizi ya shughuli zitakazofanyika kwenye Mkutano kwa kushirikiana na Wadau.

### 3.2.2 Masuala ya kuzingatia wakati wa Mkutano yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa

i. Ratiba ya Mkutano iliyowasilishwa;
ii. Uzalendo na maslahi ya nchi wakati wote wa ushiriki wa Mikutano;
iii. Maadili ya kitanzania wakati wote wa ushiriki wa Mikutano; na
iv. Mazingira ya kukuza ushirikiano na mahusiano.

### 3.2.3 Masuala ya Kuzingatia baada ya Mkutano: -

i. Kuandaa taarifa ya Mkutano na kuiwasilisha kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum;
ii. Kufanya kikao cha tathmini baada ya kurejea kutoka kwenye Mkutano; na
iii. Kutekeleza na kufuatilia utekelezaji wa maazimio yaliyotokana na Mkutano husika.

3.2.4 **Masuala mengine muhimu yatakayozingatiwa wakati wa ushiriki wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa kwa washiriki ni kama ifuatavyo;**

i. Uwazi na uwajibikaji;

ii. Uadilifu;

iii. Taaluma;

iv. Heshima; na

v. Mila na Desturi.

# SURA YA NNE: WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU

## 4.1 Wajibu wa Serikali

Serikali kupitia mifumo yake ya kiutendaji itahakikisha upatikanaji na utoaji wa taarifa ya ushiriki wa Wadau mbalimbali kwenye Mikutano. Aidha, Majukumu ya Wadau wanaohusika na uratibu na usimamizi wa ushiriki kwenye Mikutano hiyo ni kama ifuatavyo: -

## 4.2 Wajibu wa Wadau

### 4.2.1 Wizara yenye dhamana na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na makundi Maalum

i. Kuratibu vikao vya maandalizi walau vitatu kabla ya kushiriki katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;

ii. Kuwatambua na kuratibu ushiriki kwa wawakilishi wa makundi maalum yanayoratibiwa na Wizara kulingana na ajenda ya mkutano husika;

iii. Kuandaa orodha ya Mikutano ya Kikanda na Kimataifa itakayoratibiwa kwa mwaka;

iv. Kuratibu maandalizi na mawasilisho ya taarifa zitakazowasilishwa kuhusu ushiriki wa ujumbe wa nchi;

v. Kushirikiana na vyombo vingine kusimamia utekelezaji wa mwongozo huu kulingana na Sheria, kanuni na taratibu za nchi;

vi. Kushirikiana na vyombo vingine vya usimamizi na utekelezaji kwa Wadau watakaoenda kinyume na sheria, kanuni, mila na desturi za nchi;

vii. Kuratibu taarifa kwa umma kabla na baada ya kurudi; na

viii. Kuainisha vifaa au bidhaa zinazozalishwa nchini ambazo ushiriki wa nchi unaweza kuambatana nazo kama alama ya kuitangaza nchi (Zawadi za kutangaza Taifa)

### 4.2.2 Wizara yenye dhamana ya Itifaki ya Kikanda na Kimataifa itakua na majukumu yafuatayo

i. Kuratibu masuala ya itifaki ya ushiriki wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;

ii. Kupokea mialiko ya Mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayohusu masuala ya kijinsia na uwezeshaji Wanawake na kuiwasilisha katika Wizara husika; na

iii. Kutoa taarifa za ushiriki wa Wadau kwenye Wizara na Balozi za nchi husika.

### 4.2.3 Wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

i. Kupokea taarifa ya ushiriki kutoka kwenye Wizara yenye dhamana;

ii. Kusimamia utekelezaji wa maazimio yaliyotokana na Mikutano ya Kikanda na Kimataifa kwa ngazi ya Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

iii. Kukusanya taarifa ya utekelezaji wa maazimio yaliyotokana na Mkutano na kuziwasilisha kwenye Wizara yenye Dhamana

## 4.3 Majukumu ya Wadau Wengine

Majukumu yao ni kama ifuatavyo: -

i. Kuwajibika kwa Mkuu wa Mfasara wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa na kutekeleza miongozo na maelekezo yake,

ii. Kuwasilisha taarifa ya mialiko na ratiba ya Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;

iii. Kuwasilisha taarifa kabla na baada ya kushiriki Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;

iv. Kushirikiana na Wizara yenye dhamana na masuala ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum katika maandalizi ya Mikutano; na

v. Kuwasilisha programu ya shughuli zitakazofanyika wakati wa Mkutano kwa kuzingatia mpango wa Wizara/Taasisi.

## SURA YA TANO: URATIBU NA TATHIMINI

### 5.1 **Utangulizi**

Uratibu na tathimini ya Mwongozo huu unalenga kuweka mfumo wa kuratibu, kufuatilia na kuandaa taarifa.

### 5.2 **Uratibu**

Uratibu utahusisha Sekretarieti ambayo itajumuisha wajumbe kutoka Serikalini na Wadau kutoka Taasisi Binafsi. Wajumbe hao watatoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wadau wa wengine wa Maendeleo kulingana na Ajenda ya Mkutano husika.

#### 5.1.1**Muundo wa Sekretarieti**

Sekretarieti itakuwa na uongozi ambapo Mwenyekiti na Katibu watateuliwa na Uongozi wa Wizara ambao watapatikana ndani ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Mwenyekiti mwenza atateuliwa kutoka kwa wadau kutokana na ajenda husika.

#### 5.1.2**Majukumu ya Sekretarieti**

Sekretarieti itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kushauri juu ya utekelezaji wa Mwongozo;
ii. Kuandaa Taarifa ya Nchi kwa ajili ya kuwasilishwa katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa;
iii. Kuratibu vikao vya kila robo mwaka;

iv. Kuandaa orodha ya mikutano ya mwaka husika (Kalenda ya mikutano);
v. Kuitisha mikutano kama ilivyoelekezwa na Mwongozo (kulingana na Kalenda ya Mikutano ya mwaka);
vi. Kuandaa taarifa ya Mkutano;
vii. Kufuatilia utekelezaji wa maazimio.
viii. Kuandaa itifaki; na
ix. Kuandika taarifa ya utekelezaji maazimio

## 5.2 Tathmini

Tathmini itafanyika kila baada ya miaka miwili ili kupima mafanikio ya ushiriki wa Nchi katika Mikutano ya ikanda na Kimataifa. Tathmini itahusisha kutumia viashiria vinavyolenga kuonesha, utekelezaji wa mwongozo, shabaha za ushiriki wa Serikali na wadau katika mikutano, kuonesha mafanikio na changamoto.

# SURA YA SITA: HITIMISHO

Mwongozo huu utatumika kuhakikisha kuwa maandalizi na ushiriki wa Wadau katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa yanafanyika kwa ufanisi na kuleta tija kwa Taifa. Walengwa wanaohusika na utekelezaji wa mwongozo huu wanapaswa kuusoma kwa makini na kuuelewa ili kurahisisha utekelezaji wake. Ufanisi wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa unategemea juhudi na dhamira za dhati za Serikali na Wadau ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mwongozo huu utatumika kama nyenzo na dira muhimu kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Wadau wakati wa ushiriki wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa. Aidha, Mwongozo huu utaboreshwa pindi itakapotokea haja ya kufanya hivyo.